

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

CKRC

Verbatim Report Of

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, LAIKIPIA EAST
CONSTITUENCY AT NANYUKI TOWN HALL**

ON

8TH OCTOBER 2002

**PROCEEDINGS OF DESSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL,
LAIKIPIA EAST CONSTITUENCY, NANYUKI TOWN HALL, HELD ON 8TH OCTOBER, 2002**

PRESENT:

- | | |
|----------------------|-----------------------------|
| 1. Mr. Issac Lenaola | Commissioner |
| 2. Rebont Gikonera | Assistant Programme Officer |
| 3. Emma Kamunga | Verbatim Recorder |
| 4. Margaret Lesuuda | Chairlady, 3 C's |
| 5. Francis Wachira | Coordinator |

The meeting started at 10.15 a.m.

Margaret Lesuunda: Shughuli ile imetulete hapa leo ya Katiba. Wale wako inje waingie tafadhali. Tuombe. Mwenyezi Mungu, tunakuja mbele yako wakati huu tunakushukuru Bwana kwa uamuzi wako, umetuamusha tukiwa salama salimini. Tunajua kuna wale hawajaiona siku ya leo kwa hivyo Bwana, tunakushukuru pia umetuwezesha. Tunaomba Mwenyezi Mungu ili shughuli ilio mbele yetu Bwana, uwe kiongozi tukianza hadi tutakapomaliza. Tunajua kuna mambo mengi ambayo yanahusu nchi hii yetu ya Kenya Bwana, na hata zaidi Katiba ambayo inatutaliza Bwana, watu ambao wanataka kujua ukweli kuhusu maisha yao. Bwana, tunaiomba, tunaiweka mbele yako ili shughuli yote inayohusu Katiba hii na hata inayohusu nchi hii yetu ya Kenya Bwana uweze kuitazama na hata Bwana kuweza kutuongoza. Tunaomba pia wale wamekuja kuongoza hii sherhe leo Bwana, uweze kuwapakwa kuweza kuvumilia na hata kuwaza kuongoa. Tunaomba Bwana, sisi zote tunajua kile kimetulete hapa Bwana, utupe uwelewano tuweze kufanya yale yote ambayo imetulete kwa maelewano, kwa upendo, na hata zaidi Bwana, tuongane ili tukue kitu kimoja katika nchi hii. Tunaomba Mwenyezi Mungu, uanze nasi hadi mwisho. Kwa jina la Yesu Kristu, tunaomba tukiamini. Amen.

So, wananchi watukufu ambao wamefika siku ya leo, Commissioner wetu, Chairman wa Laikipia County Council, wale ambao wame kuwako mbele yetu hapa ni Commissioner Bwana Issac Lenaola, lakini tumupigie makofi kukaribisha sivyo? So, welcome Sir, I want to take this opportunity to welcome you on behalf of Laikipia East residents to today's function. I will alsothe Committee members ambao wako nje waingie ndani tafadhali ili tuweze kuwajulisha wale ambao wamefika kusikiliza mambo yanayohusu Katiba yetu ya leo. Committee members wa Laikipia East, tafadhali muingie.

Nikiwa nawasubiri, ningependa pia kuwajulisha wale ambao wameambatana na Commissioner wetu siku ya leo ambao wanasaidia. Kuna mmoja ambaye anashughulika na mambo ya Verbatim recording anitwa Emma Kamunga. Simama tu wakuone, pigia hawa makofi unajua kazi wanafanya katika nchi hii ni ngumu sana. Kuna mwingine pia ambaye ni Programme Officer ambaye ameambatana nao Bwana Robert Gitonga. Karibu sana. Nitawajulisheni pia Coordinator wetu wa Laikipia ambaye pengine hamuja muona Bwana Apolos Wachira, huyu nidy Coordinator wa hapa Laikipia. So thank you very much, I know he is also welcoming everyone. We also have his assistant na nimeona ametoka nje. Nafikiri nitachukuwa fursa hii kuruka introduction ya Committee members kwa sababu they are very busy receiving guests at the door na wengine hawajafika ili tufanye badaye, tutafanya badaye. Welcome your Worship the Mayor. Wale wengine nitawajulisha ni delegates ambao walichaguliwa hapa waende kuwakilisha Laikipia mashariki katika ile National Constitutional Conference. Delegates nafikiri kuna mmoja nimemuona hapa Bwana Joseph Schwel kutokani mmoja wale wanawakilisha. Thank you very much. Any other delegates who have arrived, wako? Tutawajulisheni baadaye.

Hata hivyo, naona Committee members wawili, watatu wameingia, I will introduce them later. I take this opportunity Bwana Commissioner, to also tell you the dignitaries who have just arrived. On your extreme immediate right is the Chairman of Laikipia County Council, tafadhali Chairman simama wakuone, Councillor Muturi, thank you very much. At the far end is His Worship the Mayor, Councillor Mathenge, thank you very much. Kuna wengine ambao wanafika hata huyo Deputy Mayor, pigia Deputy Mayor makofi. (clapping). Karibu kiti kuna kiti upande huu tafadhali.welcome, that is the Deputy Mayor of Nyanyuki, Councillor Wamae. Commissioner, kama umeona umati ulio hapa mbele ni mdogo, sio umati lakini ni watu wachache, tunaomba tu uvumilie watu wa Laikipia ni watu ambayo wanatoka mbali sana. Kuna wale wanatokanimona Councillors watatu kutoka Wasimame tuwaone wametoka mbali sana Bwana Commissioner, simama tu, thank you very much. Pigia hawa makofi wameakilisha watu kutoka mbali sana. Wengine wametoka mbali zaidi na wameweza kufika hapa, wale ambao wako hapa ni watu ambao najua pengine wametoka karibu karibu, na kuna wengi ambao watatoka hata upande wa Lamuria. Kwa hivyo yangu ni kukukaribisha wewe katika Laikipia East nakukuwambia kuwa tumetarajia sana kama watu wa Laikipia kurudishwa kwa Draft, ili tuweze kujua kama views zetu zile mulichukuwa hapa zimeweza kuwekwa ndani ama tumesahaulika.

Hata hivyo, tangu nianze kufanya introduction mimi mwenyewe sija ji-introduce, kwa majina naitwa Margaret Lesuuda, mimi ndiye Chairperson wa Laikipia East Constitutional Review. Yale tu pengine ningesema kidogo kama Chairman as my opening remarks, is when you look around the hall, you will see people spotting the yellow ribbon. We are not just sporting because we have read in the papers that people are sporting but we are sporting because sisi wenyewe tunaunga mkono, ama si hivyo wananchi wa Laikipia? Si muna unga mkono Katiba? Kama unaunga piga makofi. Kwa nini tunaunga kwa dhati mikono Katiba hii ya leo? Tunaunga kwa sababu, our resources including time, including personnel, including money which is taxed from us has been spent in billions to come up with what we can see even today as a Draft, and we should look forward to it being a complete Constitution. To every Kenyan, even those who may not understand exactly what is in this Constitution, at least you understand your feelings in your heart that as Kenyans we have seen Commissions being started and after the Commission it is very unfortunate that whatever the Commissioners come up with it is throw into a dustbin and forgotten.

So we are actually a tired group, we join other Kenyans to say that we are tired, we are no longer going to sit back and see Constitutions being made then they become useless at the end. So we are sporting the yellow ribbon on our clothes but I believe we are spotting the yellow ribbon even more in our hearts, am I right? Roho zetu ndizo zinasema zaidi ya kile yellow ribbon inasema, kwa sababu tunataka kuona hii Katiba ikifaulu. We may not understand what is inside but we understand that it is a right for us Kenyans to have a new Constitution. Some of us are almost dying of age, since we were born we have never seen new things, we want to see new things. We hope that you as Commissioners have been able to come up with new things.

So, with those remarks sitapatia wananchi waongee, leo ni siku ya Commissioner wetu kutuongoza watuambie ni nini kiliwaleta hapa. Kwa hivyo, nitachukuwa fursa hii hata kama huu si mukutano ya siasa, we want to welcome you with what we call

blessing clap because we want blessings from God, si ndiyo wananchi? Na mimi ndiyo nitaongaza hiyo blessing clap because I know they will mean a lot to us so can we start clapping. Nikisema piga, nyasha baraka unapiga polepole, nikisema bariki unapiga pa! Are you together with me? Baraka nyasha. (clapping) Mambo yawe mazuri Kenya, bariki!

Com. Lenaola: Asante sana Mrs. Lessuda, Bwana Chairman, Your Worship the Mayor, Deputy Mayor, our coordinator, macouncillor, wananchi wa Laikipia, hamujambo?(clapping) Nimeshukura sana kupata fursa ya kuja kuwa nayi leo. Na mulivyosikia mimi jina langu naitwa Issac Lenaola, namini kutoka wilaya ya Samburu. Na leo, tuko hapa kwa maana tulipokujamara ya kwanza hapa Laikipia, wenzangu walisema kwamba watachukuwa maoni yenu baada cha kuchukuwa watachambua, baada ya kuchambua watarudi tena hapa hapa Laikipia, na kuwambia kwamba yale nyinyi mulisema, yale watu wengine walisema yameandikwa katika Draft Constitution.

Kwa hivyo, tumetimiza hilo jambo. Mara nyingi Macommission zimekuja nyingi hapa. Si mumesama Commissions mia moja zimekuja Laikipia? Si nyingi sana miaka iliyopita? Lakini hakuna Commission imerudi kusema kwamba tumewasikia, tumeandika report, ndio hii report tumeandika. Hata juzi pale kortini nimesikia kwamba ile Akiwumi report ilienda ikafichwa wapi? Mpaka korti inasema toeni hiyo report wananchi wajue juu ya Akuwimi report. Kwa hivyo sisi, hii ndio report ya Laikipia East Constituency. Kila jambo mulisema iwe ni hapa, iwe ni Dol Dol, yote iko katika hili file. Ukitaka kujua kwamba maneno yako ilishikwa vizuri: mutaenda kwa coordinator, utafungua hii file usikie kama maneno yako yalishikuwa na hii Tume neno kwa neno. Sawa hilo?

Jambo la pili. Kwa Kenya zima tumezichambua hizi report kutoka kila Constituency na kuwandika hii Draft Constitution. Katiba ya Kenya mpya ambayo sasa tumewaletea nyinyi na ndiyo hiyo munashika katika magazeti. Na je, kwa maana hakuna muda mrefu, ningependa kusema hivi; hii ni Katiba ambayo iko na mambo mengi sana na kwa ashubui hii ya leo tutaweza kuenda paragraph by paragraph mpaka mwisho. Nitafanya hivi, nita- point out yale mambo ambayo mimi nafikiria baada ya kusoma hii report yenu mulisema mungetaka mambo fulani katika Katiba, nitaawambia kama kweli hayo mambo yameingia katika Katiba.

Kwa hivyo what I will do, I will only pick out certain parts which relate to what mulisema kama watu wa Laikipia wakati tulikuwa hapa. Baada ya hapo nitawapa nafasi. Kama kuna swali ama kuna jambo ambalo mungependa kuniuliza mimi kama mwana Tume, nitakupa fursa, kama niko na jibu nitakupa kama sina jibu nitakwambia sina, kama nitapeleka mbele kwa Commission nitapeleka, maanake hii Draft si final. Mumesikia Wabunge vile wamesema kwamba hiki kitu hatujui vile imetoka, ni mbaya sijui ni ya aina gani, tumesema hivi, si final. Baada ya mimi sasa kutoka hapa yale maoni yenu kuhusu hii tutayatambua tena mbele kabla ya ile National Conference to discuss that Constitution. Kwa hivyo hii na mara ya ngapi tunataka maoni yenu?

Mara ya pili. Kwa hivyo kama kuna jambo ambalo halipo nitawaambia nitapeleka wapi? Pale mbele. Tumeelewana hivyo? Ni sawa sawa? Asante.

Jambo la kwanza. Kuna wilaya katika nchi hii kama ya Laikipia, wilaya ya Samburu, wilaya ya Isiolo, wilaya ya Turkana, wilaya ya Marsabit, ambazo ni wilaya tunaita marginalized districts. Tume finywa katika hali ya Serikali, tume finywa katika hali ya kimaumbile, tume finywa katika hali ya mali, ili kwamba hizi districts si sawa na zingine. Ama nyinyi ni watu sawa na Kiambu? Muko sawa na Kijabe ni sawa? Tumesema kwamba kuna wilaya ambazo zimetengwa kando kwa sababu ya historia, kwa sababu ya mambo ya Serikali, na tumesema je, kwa hii Katiba tumesema nini kuhusu hizo wilaya? Pia, kuna watu wadogo wadogo, makabila ndogo ndogo kama Mukogodi, kama Dorobo, wale wengine wa Ogiek, je hii Katiba imewaangalia? Tuanze kufungua. Unajua saa ile ya Katiba ni kama Bibilia, kwa hivyo nikianza kufungua tutafungua vile Pastor anasemanga tufungue Chapter fulani tujue kama iko ama hakuna.

Kwa hivyo, tufungue Article 14, na kwa hii Katiba yetu tunaita Section ama hatuiti kama Bibilia, Bibilia inasema nini? Ukurasa. Hii inaitwa ukurasa ama Article? Article number 14. Article 14 ndiyo imeandika jia ya Kingereza Chapter 3. Inaandikwa National goals, values and principles. Maanake yale maadili ambayo lazima nchi hii iongozwe nayo. Article 14, pale chini kuna Article 14(2) halafu kuna Article 14(3). Kwa Kingereza nitasoma. Inasema 3, the Republic shall recognize the diversity of its people and promote the cultures of its communities. Serikali ya Kenya, ni sharti ikubali kwamba Wakenya wako diverse na watu wako wengi, makabila mengi. Na ni lazima iheshimu mila ya kila kabila. Hiyo ni taabu? Mila zetu ziheshimiwe na nani? Na Serikali. Iwe kabila kubwa, iwe kabila ndogo, iwe wilaya kubwa, wilaya ndogo, lazima mula zetu ziheshimiwe na Serikali tukufu ya Kenya.

Jambo la pili. Article 14(3). Pale chini sub article 11, chini kidogo Vice Mayor, number 11, chini ya hiyo 14(3), kuna 14(11). The Republic shall ensure the fullest participation of women, the disabled, and the marginalized communities and sections of society in the political, social and economic life of the country. Serikali ya Kenya, ni lazima ione kwamba: wanawake, walemavu, makabila ndogo ndogo na wilaya ndogo ndogo, ni lazima pia nao waangaliwe katika mambo ya kisiasa, mambo ya jamii, mambo ya uchumi. Kwa hivyo, hakuna kusema kwamba ni wale tu wengi, ni wale wakubuwa, ni wale wa kutoka Nairobi ndiyo watakao kuwa katika Serikali ama katika mambo ya nchi. Kila Mkenya atakuwa na haki ya kuwa katika mambo kama hayo.

Hapo chini, kumi na tano. Chini ya hiyo 11 kuna kumi na tano. The Republic shall promote equitable development recognize and enhance the role of science and technology, eliminate disparities in development between regions of the country and sectors of society, and manage national resources fairly and efficiently for the welfare of the people. Katika mambo ya maendeleo, Serikali ya Kenya ni sharti ione kwamba hakuna tofauti kati wilaya fulani katika nchi hii. Lazima kuwe na usawa katika mambo ya maendeleo. Kama ni barabara, barabara isiende Karbarnet na isiende Kama ni lamii ingie Bomet, hiyo lami iende Lamuria, kama lami ingie Bomet ingie..... kwa Chairman, ili kwamba maendeleo yawe sawa katika nchi zima. Ni kwamba wilaya zingine ziko na maendeleo kubwa na zingine maendeleo ya nyuma. Laikipia iwe sawa na Baringo, Baringo iwe sawa na Bomet, Bomet iwe sawa na Kisumu, ili nchi iwe nchi sawa, kila Mukenya awe Mukenya sawa popote alipo.

Haya, halafu baada ya ile 15, kuna 18. Inasema hivi 18, hapo 14(18): at least once every year the President shall report to Parliament and the nation all the measures taken and the progress achieved in realizing these national goals, values and principles. Kila mwaka Katiba yetu inasema nini? Rais wa nchi lazima aende Bunge akasema kwamba mimi kama Rais wa nchi mambo yamefanyika, hayo mambo yamesemwa katika hii Katiba yamefanyika kwa njia ifwatayo. Kwamba mambo ya maendelo yamekuwa sawa kwa nchi kwa mana ya mambo yamefanyika hivi na hivi na hivi. Hivi sasa na ni kwa heshima ya Rais na wanasisia, kuna siku President anasema kwamba kwa Bunge ama.....wananchi kwamba mali yenu ilifanya hivi na hivi? Hatupatiwi maendeleo vile yanafanyika. Unasikia ati kwamba lami imewekwa mahali fulani, maraunasikia harambee inafanyuwa mahali fulani. Tunasema hivi, sina kila mwaka Rais aende Bunge aseme kwamba nimefanya maendelo kwa nchi kwa njia fulani na fulani ili kwamba nchi nzima iwe sawa kwa maendeleo.

Hiyokwa hii Katiba? Haya, tuende Article 77. Article 77 imeandikwa chini ya election. Article 77, page, unajua sina hiyo yenu kubwa. Page 11 ya hiyo document yenu. Pages ziko tu kwa hiyo document Article 77, page 11, sub Article 2 (c). Kuna Article 2 upande kidogo halafu (c) iko chini. Mumeiona? Haya, nisome? Inasema hivi, a political party shall ensure that the remaining 50% of their seats are distributed among persons with disabilities, the youth, ethnic minorities and other interest groups. Tunasema hivi, unajua kuna vile viti vya Bunge ambavyo tunasema 90 seats ni zile za kugawa, na tunasema vile viti ya kugawa ni kama..nomination lakini system yetu si ya nomination, lakini ni kama fikiria kwa akili yako ni za kama hizi seats ni za nomination sasa si ndiyo? Tunasema hivi, 50 % za hivyo viti kama nominations iwe kwa nani? Watu wa disability, vijana na makabila ndogo ndogo, na pia watu wengine ambao wako na shida ambao hawatakuwa kwa Bunge. Kwa mfano, kuna watu wa Western, Isiolo huko pande wa kwetu huko side ya Lake Trukana, hawo watu district walihesabu wako 999 mia tisa na?

Tuseme elfu moja maana wengine wamezaliwa tangu August mpaka leo pengine ni elfu moja. Hata kama ifanyike nini wata pata Mbunge? Wata pata Mbunge kweli? Maanake kura elfu moja kwa kura thelathini elfu mutamupeleka wapi? Na wao pia wako na haki na Bunge? Mambo yao yasemekana huko. Ndio tunasema hivi kwamba vyama vya kisiasa ni sharti vione kwamba makabila ndogo ndogo pia wako na Bunge wao mambo yao poa yasikike.... katika Baringo central mahali Rais anatoka kuna kigroup ya Maasai inaitwa Njemps na pia lakini Baringo Central ni ya nani? Ni ya Watugen na hao kura yao ni elfu kumi. Kura ya Watugen ni elfu sitini Hata wakifanya nini watapata Mbunge kweli? Na tumesema pia wao wapate hiyo nafasi ya kupata mjumbe wa Bunge. Tunasema hivi, kila kabila liwe na nafasi ya kupata nini? Uongozi. Nafikiri hivyo ni vizuri.

Haya, Article 86. Article 86 (2). Hiyo ni Article ambayo inasema kwamba, wacha ni wape mfano mdogo. Miaka mwili iliopita kukaja vugu vugu huko Nairobi, kwamba kuna hizi constituencies ambazo ni kubwa sana kwa sababu ya size, kama Laikipia East. Laikipia East ni kubwa kwa size. Si ni kubwa? Na hata nyinyi ningependa ikatwe ikuwe, mlituambia siku ile tulikuja hapa tukateni ikuwe mara mbili tuu? Lakini kuna watu wakasema hivi, constituencies ambazo hazina watu wengi badala ya kukata ikuwe na constituency mbili mushikanishe. Laikipia East na Laikipia West ishikanishwa ikuwe constituency ngapi? Na je, Laikipia iko na constituency ngapi? Kwa hivyo Laikipia East ingekuwa constituency ngapi? Laikipia district ni ndogo kweli?

Mjumbe anaweza kufanya kazi ya watu kutoka mpaka Inawezekana? Ama kutoka hapa mpaka Kinamba? Si

Kinamba hii ya hapa ile ya karibu Baringo. Inawezekana? Tukasema hivi. Hata kama munaangalia mambo ya kubwa wa watu pia muangalie nini? One, means of communication. Laikipia kuna barabara ya kupeleka MP daily mpaka afikie kila mtu. Two, geographical features. Laikipia iko na hali ya anga ya aina yote sio? Muko karibu na mulima, mko mahali dry, mko mahali kama Nyanyuki, mambo kama hayo si pia yaangaliwe na Katiba?

Jambo la tatu, community of interest; ni watu gani wanaishi katika Laikipia? Tuna makabila mengi, tuna Waturkana, mko na Wasamburu, mko na Mgogodi, mko na Wakikuyu, mko na Wakalenjin, kila kabila, kwa hivyo ni vizuri kwamba constituency ikikatwa lazima haya mambo yafanye nini? Yote ya angaliwe. Si number ya watu tu, kwamba kama ni 40,000 hata kama ni namna gani basi kata constituency, na hilo ni jambo ambalo lita-affect nyinyi kama watu wa Laikipia.

Haya, jambo lingine. Article 213, mia mbili kumi na tatu, na hiyo Chairman alifurahi sana alipoona kwa sababu inafurahisha watu wake. Article 213, inaandikwa huko juu ya devolution of powers, mambo ya Serikali. Nitawapeleka 213 Sub Article 1(f), page 26, asante Mayor, page 26, inasema hivi, the principles and objects of devolution are two...1(f), ensure equitable sharing of national and local resources throughout Kenya with special provisions for marginalized areas. Inasema nini? Katika kugawa resources za Kenya lazima kuwe na special provisions for wilaya kama hii. Huwezi ku-treat Laikipia District kama Kiambu maanake resources za Kiambu si sawa na resources za Laikipia. Kwa hivyo mukigawa mambo yale tunasema national cake, mukigawa national cake mtu ambaye ameshiba kwa nini umupatie half, iko maana? Mtu mwenye njaa ndiyo umupatie nini? Hiyo nusu. Ndiyo tunasema mukigawa national resources wilaya kama hii ipewe nini? Nafasi kubwa kidogo.

Hapo chini, (i), protect and promote the interest and rights of minorites and marginalised groups. Watu wachache wachache, wale ile Commission imesema kidogo pale mbele ndogo ndogo, pia wao ufanye nini? Uangalie. Haya, pale chini, 4 Article 213 (4), the national and devolved Government shall ensure the participation of communities in decisions relating tonatural resources in their areas and the preservation of the environment. Tunasema nini? Lazima kwa mambo ya environment, kwa mambo ya mali ya asili, lazima nyinyi muulizwe kama ni sawa ama si sawa. Kwa mfano Laikipia, muko na wildlife hapa kwa forest, mko na wildlife pale juu, mutaulizwa kabla ya Serikali kuiweka ile fence ya stima waulize nani? Watu wa Laikipia. Kabla ya Serikali kusema kwamba tutafunga hii area ikue national reserve, nani aulizwe? Watu wa Laikipia, maanake natural resources, mali asili, ni yenu wenyewe sio wengine.

Haya, Article 235, samahani 225, page 27, hiyo page next, Article 225 Sub Article 3, inaongea mambo ya fedha. Wale ambao wako katika Serikali na wale wengine ambao munafanya kazi munajua kama kila mwaka kuna grants ama pesa zinatoka Central Government zinakuja wapi? Katika district, si kunazo hizo pesa? Katika 225, 3 (c), tunasema there kwamba grants shall include equalization grants paid to marginal districts. Grants za usawa, kusawazisha mawilaya. Huwezi pea wilaya ambayo iko na barabara ya lami ten million na ile ambayo haina lami munaipa ten million, maanake ile iko lami si inapiga hio lami ya juu tena na huyu mwenye hana lami anaanza na nini? Scratch. Tunasema ya kwamba fedha za Serikali zipewe nyingi kidogo kwa wilaya kama hizi kama Laikipia ili kuwe na usawa na wilaya zingine. Iko makosa hapo? Kusawazisha wilaya kuna

makosa?

Haya, hapo chini Article 226, inasema hivi. Districts shall be entitled to a substantial share of the national revenue from local resources and for the allocation of a fixed percentage to the communities in whose area the resources are granted. Tulipokuwa hapa mulituambia na iko kwa report yenu, tungenda kwamba fedha zikitoka Laikipia 80% ibaki wapi? 20% iende wapi? Nairobi, na tumesema hivi, percentage kubwa ya national resources ibaki katika? Katika wilaya. Isiende kwa Central Government.

Article 239, samahani Article 235 page 28, number ya mashamba. Tulipokuwa hapa Laikipia tuliwaambia hivi, tulisikia hapa Nanyuki, tukasikia hivo Mgogodo, kwamba Laikipia district sio ya Kenya tena. Laikipia ni ya nani? Ya wazungu. Maanake wanakuja watu ambayo hawana citizenship ya Kenya wanachukuwa titles ya land ama leases ya land kwa miaka mia tano na tisa. Hata kuna wengine wako na land leases for 999 years, munajua hiyo watu wa Laikipia? Tunasema hivi.

Article 235, Sub Article B(2), inasema hivi: that within two years of the coming into force of this Constitution, Parliament shall review and assess all claims to unjust (inaudible) of land in the Coast, North Eastern, and Rift Valley Provinces or elsewhere arising from historical or other causes in order to establish their validity and how best they can be justly, peacefully and equitably resolved. Kwamba Bunge, miaka mbili baada hii Katiba kupitishwa kama itapitishwa kwa sababu hiyo ni story ingine, lazima kuwe na sheria kwamba hizo claims kama hizi za Laikipia, kwamba mashamba yalichukuliwa kwa maana wazungu walikuja hapa 1895 wakajipatia mashamba baada ya kulipa one pound, na sasa baada ya miaka mia mmoja mtu moja ako na acre eighty thousand, a hundred thousand, two hundred thousand, na Wakenya wa..... hawana nini? Hawana mashamba. Tunasema lazima Bunge ifanye sheria in the next two years kwamba hizo claims iwe ni hapa ama Coast ama North Eastern, zikuwe resolved ili Wakenya wapate benefits zao. Jambo lingine ni kwamba mambo ya hizo leases, milioni hapo mambo ya leases kwamba hizo leases zitakuwa reduced to 99 years.

Article 233, Article 233 just make...on page 28, inasema, subject to this Constitution no person other than a citizen of Kenya shall have the right to acquire any interests or rights in land in Kenya. Hakuna mtu ambaye si Mukenya ambaye hana cheti cha kuwa Mukenya, atakuwa na nini? Haki ya kuwa na ardhi wapi? Katika Kenya. Tukasema hivi. Hapo chini Sub Article 3, no citizen of Kenya may hold or use land on the basis of lease of Kenya only, and such leases shall not exceed 99 years. Ukiwa si Mukenya na ungependa kutumia ardhi katika Kenya, huwezi ukaja kupata lease ya miaka elfu moja ama miaka elfu kumi ama mwaka hata elfu mia moja. Limit ni miaka mingapi? 99 years.

Haya, Article 243, page number 29, hii ina-deal na mambo ya finance, fedha za Serikali. Article 243(c) inasema, the Serikali shall ensure equitable sharing of national and local resources throughout Kenya, taking into account the special provisions for marginal areas. Kwa hivo kugawa finance ...kwanza, kugawa revenue ya Serikali lazima kuwe na kuanglia wilaya kama hii. Nikimalizia, mambo ya wilaya kama hii, mumeona kwamba mulituambia katika wilaya ya Laikipia mambo matatu nikikumbuka.

Jambo la kwanza- mambo ya mashamba, jambo la pili-mambo ya national resources, jambo la tatu-mambo ya usawa wa wilaya. Kwamba lazima wilaya kama hizi zipewe mambo fulani kidogo, what in English we call Affirmative Action, muongezewe fedha, muongezewe maendeleo ndiyo mukuwe sawa na wilaya zingine. Hayo yote nimewasomea yameingia katika Draft ya Katiba hii.

Haya, wacha niende mambo ya land....., Article 232. Article 232 inasema hivi. Land being Kenya's primary resource and the basis of land use for the people of Kenya, shall be held, used, and managed in a manner which is equitable, efficient, productive and sustainable. Kwamba ardhi ya Kenya, maana ndiyo rasilimali kubwa katika nchi, lazima itumiwe kwa usawa na nchi, kwa uzuri, na ili kwamba iwe productive na iishi kwa muda ambao unakuja. Mashamba isitumiwe vibaya lakini itumiwe kwa nyaba ya watu wa Kenya. Article 234, inasema tofauti kati ya mashamba ambayo ni yangu binafsi, mashamba ya group na mashamba ambayo si ya group. Na wakisema hayo utajua difference kati ya community lands na pia lands ambazo ni private. Lakini kwa ndugu zangu kutoka Mgogodo maanake hawa wako katika community lands hebu tusome Article 235, Sub Article 2(b), the same page, Article 235 2(b). Community land shall not be disposed of or otherwise used except in terms of the legislations certifying the nature and extent and the rights of members of each community, individually and collective. Nasema ambayo imesema isipeanwe bila sheria ya kusema vile itapeanwa.

Haya, ...ingea kidogo mambo ya security, maanake Laikipia shida yenu kubwa baada ya mashamba ni nini? Na je Katiba inasema nini juu ya security yenu katika wilaya hii? Turudi nyuma kidogo. Article 41, page number 7. Page 7 ya hii Draft Article 41 pale chini inasema, freedom and security of the person, every one has the right to freedom and security of the person which includes, kila mtu ako na haki ya kuwa-security inasemwa aje kwa Kiswahili, usalama? Usalama wako mwenyewe na ya kwanza ni kwamba not to be deprived of freedom arbitrarily or without just cause. Yaani huu usalama usichukuliwe kiholela holela ovyo ovyo? Jambo la kwanza.

Jambo la pili, not to be detained without trial, usifungwe bila nini? Bila kusikizwa mahakamani. (C), to be free from all forms of violence from either public or private forces. Uwe free, ile group isije ikakuchapa ama pia mtu mmoja asije akakufanya nini? Na tena unasikiza hii ndiyo kitu ambacho malikuwa mnataka sana. Kwamba tuwe na haki yetu kwamba group fulani isije ika-attack group nyingine ama mtu fulani, asichochee wengine ku-attack watu wengine kwa sababu nyinyi ndiyo mumepata brunt ya clashes sana sana 1997. Na tumesema kwamba kuwe na hiyo haki. Nitawaeleza baadaye kama hizi haki zilikivunjwa mutafanya nini. Kwa hivyo mumesikia ni kwamba ukipeleka tu bila kuwa na mechanism ya ku-enforce.

Halafu (d), not to be tortured in any manner whether physical or psychological. Usinyanyaswe kimwili kwa njia yoyote. (E), not to be subjected to corporal punishment or to be punished in a cruel, inhuman or degrading manner. Usidhulumiwe, usifanyiwe unyama na mtu yeyote. Article number 43, hapo chini tu kidogo: privacy. Every person has the right to privacy which includes the right not to have their person or home searched. Hapa Laikipia tuliambiwa tulipokuja kwamba polisi wakija kwako nyumbani hawakuji na warrant. Unasikia tufungua, polisi inangolewa. Tumesema sasa hakuna mtu kuingia kwako ama

mali yako ama mfuko wako bila kuwa na nini? Warrant. Maanake polisi wakushika hata bila kujua jina lako nani anaingia hapo? Kuona kama kuna mali donde usiku umeweka pale kando. Tumesema hiyo itakuwa nini? Ni hatia, ama Article 43 (c), their possessions seized Anti Stock zinakuja siku hizi kutufwata kama watu wanaiba ngombe, hakuulizi kama ngombe hii ni yako ama imeibiwa wanafanya nini? Si wanapatia tuu? Tumesema hiyo ni hatia.

Haya, Article number 54, page 8. Sorry, page 9 pale chini, every person has the right to acquire and own property either individually or in association with others. Haki ya kuwa na mali yako iwe ni binafsi ama uwe ki-group.(interjection inaudible). Anasema ako na kazi anaomba kwamba aende tumkubali afanye kazi ya kujenga taifa. Asante Chairman. Haya twende huko nyuma kabisa Article 264. 264 ni page number 32. Page number 32 Article 264, mulituambia hivi mambo ya polisi, kwamba Katiba ya Kenya iseme jambo fulani juu ya polisi maanake siku hizi hatujui kama polisi wanaelewa kazi yao ama hawaelewi. Mukatwambia nyinyi, mukatwambia mutuandikie “je, kazi ya polisi katika Kenya ni nini, ili sisi tujue na pia hawa wajue”? Kazi ya ni kuwafanyia wananchi kazi kwa njia zifwatoazo: Jambo ya kwanza kuona kwamba there is a peaceful and safe environment. Kuona kuna nini? Amani katika nchi. Jambo la pili, protection of rights and freedom. Kuona kwamba haki za watu zinakuwa protected. Jambo la tatu, prevention and detection of crime, wakiona makosa wanayakataza ama watueleze. Jambo la (c), the security of the people, usalama wa? Wananchi. Kwa hivyo sisi zote tunajua na polisi wanajua kwamba katika Katiba mpya shughuli zao ni hizo ambazo ziko katika hapo. Mambo ya security tunaweka katika Katiba hii.

Haya, na mlizungumuza juu ya ufisadi, corruption, mulituambia Kenya imejaa corruption tungetaka mufanye jambo fulani kwa Katiba ili corruption imalizike. Kwa hivyo tuingie mambo ya? Corruption. Inasema nini hii Draft juu ya corruption. Article number 14, pale nyuma, page number 5, I believe. Article 14, Sub Article 6 is page number 5, page number 5, Article 14, sub article 6 inasema hivi: “ the republic shall take effective measures to eradicate all forms of corruption”. Serikali ni lazima ione kwamba ufisadi unafutwa, na je itafanya hivo kwa njia gani? Nitawapeleka mpaka Article 2, 89, Article 2 (89), ni Commission ambayo inaitwa Ethics and Integrity Commission. Hii ni Commission ambaye kazi yake imesemwa hapo. Kazi yake moja ni page number 36. Page 36 sub article (j), the Ethics and Integrity Commission, kazi yake moja (j), investigate instances of corruption. Hii ni kama ile Kenya Anti Corruption Authority na tunaita hapa Ethics and Integrity Commission, kuona kwamba mambo ya ufisadi yanakuwa investigated.

Jambo la maana zaidi, munaona pale nyuma katika hii document kuna page number 45. Munaona hapo inaandikwa leadership and integrity code of conduct, mumeiona hapo? Katika hii document yote, katika hiyo draft nzima karibu kila ofisi iwe ni President, iwe ni Prime Minister, iwe ni Vice President, iwe ni Wabunge, iwe ni ma-judge, iwe Attorney General, wale ma-councillor, kila mmoja ni lazima afuate hii inaitwa leadership and integrity code of conduct. Kama huwezi kufwata masharti ya hii code atolewe katika kazi. Kwa mfano, kama Prime Minister akichaguliwa na ionekane kwamba amekataa ku-declare pesa zake ama mali yake na mahali hiyo fedha na mali imetoka, atakuwa disqualified, kuwa nani? Kuwa Prime Minister. Kama MP akiambiwa atueleze ako na Mercedes tatu, uko na lorry tano, uko na nyumba kumi, uko na buildings ishirini Nairobi, kumi Nyanyuki, tano Nyeri, aseme alitoa wapi zote na asiposema mali ametoa wapi atakuwa disqualified kuwa nini? Prime Minister,

ama Minister, ama MP.

Kwa hivyo kama kuna suspicion kwamba hii mali ni ya ufisadi unafanya nini? Unagatuka kama vile Nyerere alikuwa anasema unangatuka kwa ofisi. Katika hiyo code of conduct, nitawasomea tu moja, tusome number 8, the following are serious offences which are in conflict with the leadership and integrity code. Number (b), misappropriation of the funds of the public office or destruction of property of public office. Kama wewe story yako ilikuwa ya kuingia katika parastatal na kunyoa ama kuingia katika council na kunyoa, baadaye utaonekana kama wewe huwezi kuwa nini? Kiongozi katika hii sheria mpya ya Kenya. (c), engaging in a corrupt practice or seeking or accepting a bribe for performing or not performing a duty or a task. Kama wewe mfiisadi umezoea kwamba katika kila ofisi ukonayo ukona kabahasha hapa chini ya kuwekewa rushwa hutakuwa kiongozi katika? Nchi hii. Number 8, deliberately disrupting meetings and interfering with the orderly functions of a public office or institution. Kuna watu ambao tunawajua ndani ya Kenya, kazi yao wanasema ni viongozi, lakini kila mkutano akiingia lazima kuwe na nini? Na violence. Wakiingia mkutano fulani hawaingii na heshima kwamba kuna secretary ama kuna nani anaingia na kifua, huyo mtu hawezi kuwa kiongozi katika hii code.

Jambo lingine hapa, tumesema kwamba hakuna mtu ambaye ako katika ofisi kuu atakubaliwa kuwa na fedha katika account za ngambo. Umesikia wakati.....kwamba pesa zetu hazikaa hapa, zinakaa wapi? Switzerland, Germany, (inaudible) Islands, Isle of (inaudible), billion na mabillion. Mujue hili watu wakipeana contract pesa hazikuji hapa, zinaenda wapi? Zinaenda ngambo, tumesema kila Mkenya ambaye kutoka kwa Deputy Secretary mpaka President, fedha zao zikuwe wapi? Zikuwe Kenya, ili kwamba ufisadi na corruption usikuwe encouraged na kuwa na account ambazo fedha zinafikia huko nje na hazikuji hapa, tujue kama zimefika ama hazijafika. Tumejaribu katika hii draft kuona kwamba corruption inakuwa eradicated.

Haya, Je, muundo wa Serikali ambao uko hapa ni wa aina gani? Nitawapeleka Article 213, page number 26. Samahani kwa maana nawapeleka mbele na nyuma maanake yale mambo ninataka kuyazungumuza hayako mahali moja na hiyo ndiyo hali ya Katiba, lazima mambo yashikane ndiyo ujuwe kwamba kila kitu kiko hapa; lakini hii ya Serikali iko mahali moja tu. Tulipokuwa tukizunguka kutafuta maoni tuliambiwa, hatupendi kwamba, jambo la kwanza, Serikali iwe mbali na sisi, kwamba ukitaka passport, title deed, upande wangu mwenyewe, nikitaka kuona mkubwa, fulani mambo ya land yote iko wapi? Nairobi. Tunataka Serikali iwe karibu na sisi. Pili, hatungependa kuwa mtu ambaye ni wa kuongoza kiti iwe ni Chief, iwe ni DO, iwe ni DC ama PC, ni watu ambao wakija kuwachagua. Tukasema ati je, ni Serikali ya aina gani ambayo itafanya Wakenya waone kwamba viongozi wao ni watu ambao wameshikana nao katika mambo ya maendeleo.

Tukasema kwamba, one, Serikali ya karibu zaidi iwe katika wilaya, iwe katika? Wilaya. Na je, katika wilaya kuwe na Serikali ya aina gani? Tunayo district council, kutoka hapo twende wapi? Kwa Kenya nzima tumeambiwa hawaoni sababu kuwe na divisions. 90% ya maoni juu ya divisions imesema kwamba division ifanye nini? Ikuwe scrapped. Maintain district, maintain location na kutoka location muende wapi? Vijiji. 90% ya Wakenya walisema hivyo na tukaona kuja kukataa ku-implement haya maoni itakuwa makosa kwa upande wa Commission maanake tuliambiwa nendeni mukawasikize nani? Wakenya. Na

Serikali hii yote tunaweka hapa ni vile mulisema, kuwe na districts, kuwe na location na kuwe na? Villages. Na je, sasa district katika Katiba hii ni district gani? Tukasema tukianza juu ati boundaries za district mutakuwa na msukosuko. Na pale nyuma tumeandika kwamba hizo districts zote ambao ziko sasa, 70 of them, ziwe district katika Katiba hii. Pili, what is a village? Maanake kijiji, Tanzania wako na vijiji ambavyo vilianza tangu independence lakini Kenya ukienda Mgogodo ni ngumu kujuwa hiki ni kijiji ama si kijiji maanake saa hao wanahamama..... ni mobile kijiji ama kitu ambacho kiko? Tukasema hivi, kijiji ni sub-location, what we are calling a village here is what we know today as a sub location. Kwa hivyo Serikali ni Serikali ya sub location, location, na wilaya.

Article number 216, page 26, the village decides whether the council is constituted by village elders or civil election. Katika wilaya nyingi tunayo tumeambiwa kwamba kuna wazee wa vijiji kwa Wabaluya wanaitwa Liguru, kwa Wakikuyu wanaitwaje wale wazee wa kijiji? What are they called? Wale wazee wanaitwa nini wale wazee ambao wanakaa na Sub Chief? (inaudible interjection). Tukaambiwa tungependa kwamba village council either iwe ni sub area wale wazee ambao tunawajua ama tuwapigie kura. Tukasema hivi, kila kijiji iamue, sub location iamue kwamba watu wetu ni sawa ama si sawa. Kuna wengi ambao munajua ni walevi, ni watu ambao wanakula rushwa, tunajua hiyo, na tungetaka nyinyi wenyewe muamue mutawapigia kura ama tuta-appoint wazee ambao tunawajua. Kuna wazee ambao kila kipindi wanajulikana. Mutaamua hiyo.

Halafu 217, the location consists of two reps elected by each village council from among its members. Kila sub location ikiwa na members sita wataamua ni wangapi wawili wataenda wapi? Wangapi? Wataenda kwa location. Wangapi? Katika every sub location wataingia katika location kwa ile council ya location. Na je, kutoka location wataingiaje katika district? Article 218, number 2, the district council consists of a member elected by the voters of the district. The council shall consist of not less than twenty or more than thirty members. Mutachaguwa moja kwa moja district councillors thelathini ama ishirini, wakuje kwa district council. Tumeelewana hapo? Mumeshika hiyo kwanza? Councillors thelathini ama ishirini kura moja kwa moja kwa kisanduku wakuje mpaka kwa district council. 218, mambo ya authority ya councillors sasa, mambo ya authority ya district commissioner sasa tumeyashikanisha, munaelewa hiyo? Councillors na DC watakuwa sasa kitu kimoja katika district council na DC hataitwa tena DC ataitwa at Article 218 (3), the district administrator, DA,. Na huyu DA atateuliwa ama atachaguliwa? Article 218 (4). The District Administrator is elected directly by the voters of the district.

Sasa yule DA ambaye atakuwa Executiveto a district atapewa kura moja kwa moja na wilaya nzima. Haya, na je, wafanyakazi wa wilaya nani ata wateva? Article 218 (5). Huyu DA hata-appoint Chief Officer wake lakini council mpaka ifanye nini? I-approve. Akitaka water engineer ana-appoint lakini council itafanya nini? Akitaka district works officer ana-appoint lakini council wafanye nini? Ili kwamba hawa elected leaders ndiyo wanaamua nani atafanya kazi yao. Munajua kwamba sasa hivi ma-councillors hawana nguvu juu ya clerk unajuwa hiyo? Kwa sababu clerk anatoka wapi? Nairobi. Tunasema kwamba all chief officers of a district, wacha huyu DA aseme kwamba nimefanya interview the following are my candidates. Council iketi iangalie waone kwamba huyu ha-qualify, huyu ni corrupt, huyu ni mkora, halafu wale ambao wanapitishwa wanapitishwa na council.

Haya, na je, huyu DA akianza kumea pembe kwa vile yeye ni accounting officer yeye ndiye mdosi katika district, je, hii council itamufanya nini? Tunasema hivi Article 6, the District Administrator can be dismissed by the vote of an accrued majority of members of the district council supported by referendum by a majority of those voting in referendum. Huyu DA pia yeye ma-councillor wakiamuka ashubuhi waone kwamba tumfute nani? Huyu jamaa, hapana, tunasema hivi, watapiga kura kwamba tumfute huyu DA wetu lakini pia nao wawe na nini? Over 50% ya councillors, baada ya kufanya hivo watalete kwa referendum, kura ya maoni, kwa wananchi, maanake wakati mwingine pengine councillors hawana sababu ya kufuta nani? Huyu DA na pia wananchi wanamupenda huyu DA. Tunasema kwamba wananchi pia wapate nafasi ya kupiga kura ya kwamba huyu DA ni mkora aende ama asiende. Hii ndiyo inaitwa checks and balances, kwamba kusiwe na mtu mmoja ambaye ni powerful katika district, kuna balance na pia wananchi wana nafasi ya kuona uongozi wao inaenda barabara.

Na je, Serikali ya province ni Serikali ya aina gani? Article 219 (2), the provincial councils consists of two person one of whom shall be a woman chosen by each district council from among its members. Serikali ya province, kila wilaya itakuwa watu wangapi? Wawili. Moja mwanaume moja mwanamke, wapeleke hawa kwa province, na province katika (3), hawa ma-DO wote, ma-district administrators, watkuwa executive council ya province, kazi yao nikuona kwamba mambo ya maendeleo katika province, yale ambayo inashikana yanaambatana na wilaya moja kwa moja. Article 219 (3). Hapo kutakuwa na mmoja wao anaitwa provincial administrator na atakuwa anaagalia mambo maendeleo ya katika hiyo province. Kwa hivyo mumesikia vile nimeongea sasa watu wanasema kwamba tumengoa provincial administration, tumengoa district admistration, tumengoa locational chiefs, hatujawangoa, tume wa reform.....ili kwamba wananchi wawe na nguvu ya kuwachagua na pia ya kuwa,ile ile tu, lakini they are more accountable to the people now, not just the President but to the people and to the electors.

Haya, Article 220 inawaambia mambo ya Serikali hizo, mtasoma wenyewe. Lakini mtaniuliza je, tuko hapa katika Nyanyuki municipality, Nyanyuki si location, Nyanyuki si district, municipality sasa, tuta itaje?. Samahani, Article 222, Nairobi itakuwa territory ya capital territory. Kama Nairobi haitakuwa district, ama province ama location, itakuwa tu national capital. Na kutakuwa na sheria fulani tulitunga kuchunga Nairobi peke yake. Pili, a city or municipality has the status of a district. Kwa hivyo kuna Mombasa city, kuna Kisumu city na kuna mahala kama Nyanyuki municipality. Tunasema hizo ziwe kama district maanake Municipality na city ni kubwa sana. Nyanyuki sasa tuki-compare economy yake ni kubwa sana sio? So, municipality, city inakuwa kama district. Na je, what about towns and urban centers. Kuna zile towns na urban centers katika sheria ya sasa. Tumesema hizo ziwe kama location.

Mambo ya finance iko katika 224, na mara ya kwanza nilikuwa nasema kwamba kuna hizo grounds na vile ya kushare resources kati ya districts na national Government. 226, sharing of national resources. Vile ya kugawa mali katika district, na province, na pia nation.

229. Kama wilaya ya Laikipia inataka kufanya maendeleo yake na wilaya ya Samburu tumesema ni sawa. Wanapanga

programme yao pamoja maanake kuna, tusme kama mambo ya barabara. For example kati Laikipia ya Samburu, ama Isiolo na Laikipia, barabara ifike border ya Laikipia na isiendeleo mpaka wapi? So, programmes ambazo ziko joined lazima ziweko hapo. Kwa ufupi hayo ndiyo mambo tumeweka katika Serikali, muundo ya Serikali. Mengi yako katika hii document muyasome tafadhali.

Haya, mambo ya Bunge, Parliament. Samahani sasa sauti inaanza kunipotea, Article 101. Article 101 page number 14. Article 101 pale juu. Kutakuwa na vyumba viwii vya Bunge. Wale ambao walizaliwa kabla ya uhuru kama hii generation yetu ya uhuru generation kulikuwa na vyumba viwili. Kulikuwa na lower house na senate. Tunasema hivi, to retain ile lower house sasa, vile iko Bunge, wa sasa, 210 constituencies ikuwe lower house. Lakini pia kuwe na upper house maanake hii lower house kwa miaka arubaini imeanza kuwa haiendi straight. Maanake haina mtu ambaye inaambia Bunge, siku hizi nani anaambia wabunge kwamba wamefanya makosa? Hakuna maanake hawa ni authority unto themselves. Wakipitisha bill hawaulizwi haulizi. Tukasema hivi, kuwe na district council, Article number, sorry, national council, Article 106. Kila wilaya ichague watu wangapi? Delegate moja, MP moja aende kwa upper house lakini delegate huyu wa upper house asikuwe tu MP kama yule wa chini. Tukaseme tumuongezee nini? Miaka. Maanake, ningetaka wazee waketi katika upper house. Kwa hivyo lower house MP anaweza kuwa from 21 years and above. Ukiwa 21 years una qualify kuingia lower house, national assembly.

Ukiwa 35 years and above ambapo umekaa kidogo unaigia kwa upper house. Unaelewa hiyo? Na je, kazi ya hao ni nini? Lower house inatunga sheria. Zile sheria za Kenya moja kwa moja. Lakini upper house mpaka ifanye nini? Ione kwamba ni sawa. Check kwa lower house. Inaangalia kwamba lower house isifanye makosa kutunga sheria ambazo ni sawa, na pia hapa tunawaambia vizuri sana lower house itafanya nini, upper house itafanya nini.lakini hiyo ndio structure vile nimesema sasa.

Na je, cabinet, mawaziri, watakuwa wakitoka Bunge? Tumesema hivi, hapana, maanake tumeona kwamba mbunge akikuwa pia waziri hafanyi kazi ya waziri vizuri, na hafanyi kazi ya MP vizuri. Anagawanya. Ni wape mfano moja, tulienda Mwatate constituency na hii niliambia Mwehismiwa Madoka hawezi sema nimemusema vibaya Nyanyuki, Mheshimiwa Marsden Madoka ni mbunge wa Mwatate lakini pia ni Minister for Foreign Affairs. Wakasema hivyo hapo Mwatate na alikuwa hapa yeye mwenyewe. Tungetaka kwamba mbunge askiwe tena nini? Waziri, kwa sababu huyu tangu akue Foreign Affairs Minister hatumuoni sisi, tunasikia ati ako wapi? Ngambo. Kwa hivyokazi ya Minister na kazi ya MP. MP akue kazi yake peke yake ni MP na waziri akue kazi ya? Waziri. Ili kila mmoja akue efficient kwa kazi yake. Ukigawa kazi.....? Tukasema kwamba Ministers itoke nje ya Parliament lakini wakuje hao ma-Minister waseme nini kwa bunge? Waseme mambo ya Serikali kwa Bunge, watakuwa kama Ex-Officio members of Parliament, waseme kwamba Serikali ifanye hivi na hivi na hivi, Wabunge wamuulize hapana hatukuona hiyo maendeleo sisi.

Na je, Prime Minister? Prime Minister atakuwa amechaguliwa kutoka Bunge ili akuwe kati ya Bunge na Serikali. Munaona hayo maneno? Prime Minister ni Mbunge na pia ndyo mkubwa wa Serikali etc. Na yeye atakuwa akija kila siku kuongea

kwa Bunge kusema kwamba Serikali yangu na fanya hivi na hivi na hivi. Serikali kama ya UK, unaona hiyo Serikali ya UK kwamba Tony Blair huenda kufanya nini? Kuenda kwa Bunge. Nimeanza kuchoka sauti. Nikimalizia jambo la misho. haki zenu kama wanainchi, je, muna haki gani? Fundamental rights. Article number 29 page 6. Ukiwa Mukenya uko na haki gani? Kutoka Article number 29 mpaka Article 75, Article karibu sitini zinaongea juu ya haki zenu. Kwa mfano, Article number 35 on page number 6, haki za wanawake. Article 36, haki za wazee, wote ambao wamezeeka katika nchi. Je, kuna haki gani ambazo tumewapa? Hizo ziko hapa. Article 37, haki za watoto wetu. Article number 38, the family. Haki za jamii ziko wapi? Article 44 page 7, haki ya kuabudu.

Na hapo nitaongea jambo moja lililokuwa ngumu katika Tume. 99% za Wakenya walituambia, mlituambia kwamba kuna haki ya kuwabudu na watu huabudu shetani. Ama mlituambia tuwe na haki ya kuwabudu na kila mtu awe na kanisa yake kama sasa. Niwaambie ukweli, hili jambo peke yake, hii mambo ya freedom ya worship ilichukuwa nine hours ku-debate, masa matisa ku-debate, hii peke yake. Tukaamua kwamba vile tumefanya, kwa sababu ukiniambia mimi sasa, kuna watu ambao (inaudible) ukiniambia uko na haki ya kuwabudu lakini abudu Mungu peke yake, hiyo haki si umenipatia na umechukuwa? Ama niambie uko na haki ya kuwabudu lakini uabudu Mungu ya Kikristu na Kiislam peke yake. Je, kama mimi ni Muhindi? Ama uniambie uko na haki kuwabudu lakini lazima uabudu kitu fulani. Najua watu kama Leakey ambao hawaabudu kitu fulani. Kama hii iko kwa kisheria it is a very difficult part of our work, how to frame these rights kuona kila mtu amefurahi Katiba vile imefanywa.

Haya, Article 45, haki ya kuzungumuza. Ile ambayo lazima itawachekesha kidogo ni Article 49. Article 49 on page 8. Every person has the right peaceably and unarmed, bila silaha, without the requirement of prior permission, bila licence, to assemble, kukutana to demonstrate..... Kuandamana, to demonstrate, to picket and to present petitions to public authority. Tuliambiwa kwamba hatutaki kwamba nikitaka kuwandamana lazima niende kwa polisi wanipatie nini? Wanipatie licence, lakini hii ikiwa italetwa najua mutasema na je, kila mtu aamuke aende apige demonstration yake bila permission lakini hii pia ilikuwa na (inaudible) kwa Commission lakini mutawambia kama ni sawa ama si sawa.

Article number 53. Haki ya kuwa na kazi. Halafu Wakenya walisema hivi, page number 9, Article 57, tunataka haki ya afya, the right to health. Hiyo iko, haki ya elimu. Article number 58, haki ya manyumba, housing. Article number 59. Article number 60, the right to food, haki ya chakula. Article number 61, haki ya kuwa na maji safi. Article number 66, every person has the right not to obey unlawful instructions. Marakwet walisema kwamba mtu akija maanake Police akuwambie kwamba vua nguo kwa sababu yeye ni Police, hiyo ni lawful? Ni sheria nzuri? Kwamba uvue nguo? Tukasema amri kama hiyo si amri ya sheria na uko na haki ya kukataa.

Article number 68. Haki za watu ambao ni wafungwa. Tumesikia mara nyingi kwamba mtu akishikwa ananyanyaswa, anafinywa, hana haki atembelewe na watu wake, hapatiwe chakula, hizo haki zote tumeziweka hapa, mpaka Article number 69. Mambo ya kortini. 69, Page 10, the right to a fair trial. Haki ya kuwa na mahakama ambayo inaku-try kwa kihaki. Je,

